

## **2 Wakorintho 4**

**Katika mlango huu,Paulo anaonyesha kujitolea kwake kwa injili na kushiriki kwamba mwanga wa injii utang'aa kupitia kwa maisha ya waamini,pasipo kujali mipango ya adui.Ingawa kuna udhaifu wetu wa kibinadamu,yeye ameshawishika kwamba,kupitia kwa vyombo vidhaifu vya kibinadamu,maisha ya Kristo hushinda nguvu za mauti.Mara tena anaongea kwa ujasiri juu ya ukuu wa utukufu wa milele unaokuja,unaotuwezesha sisi kuinuka juu ya changamoto ambazo tunamenyana mireka nazo katika maisha haya.**

### **Huduma ya Agano Jipya**

Ni huduma inayopeanwa kwa neema ya Mungu,kumtangaza Kristo kama anayeleta njia mpya kuenda kwa Baba.Paulo amejitolea kuhubiri neon la Mungu bila kulegea au kujadiliana.Ulimwengu hutafuta kupitisha ujumbe wake kwa kutumia njia zote za kueleweka,njia za udanganyifu lakini hatuhitaji pia kutumia njia hizo.Wahuduma wa ukweli wa injili wako na hisia au dhamira iliyo wazi.Tunashiriki kwa unyenyekevu ukweli na kuwahimiza watu wasawazishe mambo yao na Mungu.

### **Injili iliyofunikwa**

Ukweli kwamba Kristo alikuja,akafufuka kutoka kwa wafu,na siku moja atarudi,kwa watu wengi,imefichwa kutoka kwa mioyo yao.Injili ni kweli lakini inaonekana isiyo ya uzima mpaka huo ufunuo unaotoka kwa Mungu,huja juu ya nafsi sinazo amini.Paulo anasema kuwa ibilisi amewapovusha watu kutoona nuru ya injili.Ni fursa kubwa ya ajabu kwetu sisi,ambao mwanzo tulikuwa vipovu lakini sasa tunaweza ona jinsi vile Bwana anatupenda sisi na kwamba amejitolea mwenyewe kwa ajili yetu sisi.Kwa hivyo wengi wa Wayahudi hawangeweza kumuona Kristo kama Masiya.Hata hivyo,kwa sababu Paulo alijua kuwa Kristo amefungua macho yake,aliamini kuwa Kristo pia atafungua macho yaw engine.

### **Injili ambayo tunatangaza**

Hii injili sio injili yetu lakini ni injili ya Bwana.Sisi ni watumishi wa Yesu Kristo.Yeye ni Bwana.Yeye ni Mungu aliyefanyika mwanadamu kwa ajili yetu.Yule aliyenena wakati wa uumbaji na kuleta nuru kwenye kiza,anataka kunena katika maisha yetu ya kiza ya Kiroho na kuleta nuru yake.Paulo kukuzia uso wa Yesu ni ya muhimu sana.Angalia maelezo ambayo Yohana anatoa katika(Ufunuo 1:16).Uso wa Yesu ni nuru,ni ya utukufu,ni ya nguvu kupita kiwango lakini siku moja,tutamuona uso wake na kumuabudu Yeye.

### **Udhaifu wa wanadamu na kudhulumiwa**

Hizi changamoto zote huleta madhara.Picha ya Paulo ya vyombo vya udongo unachochea fikkra.Vyombo huwa na dhamana kuu lakini ni vidhaifu.Hata hivyo,Paulo haoni hii kuwa ni ya kinyume kabisa lakini,mbali, hufurahia kwamba nguvu na utukufu wa Mungu unaweza kuonekana,licha ya udhaifu unaonekana.Kuelezea kwake juu ya mateso ya waamini,yaweza kuwa ya kutisha,kama haike kuwa kwa ujumbe ulio wazi kuwa kuumia na kudhulumiwa uliokuwa pia sehemu amayo Yesu alipitia.Yesu yuko na sisi na atatipitisha kwa hayo mabonde ya kuumia na kudhulumiwa.Yesu alifufuka kutoka kwa mauti na atatipitisha kwa usalama kwa hizi thoruba za maisha ili tuwe naye milele.

### **Udhabiti wetu ndani mwa Kristo**

Paulo yuko na uhakika kwamba mwokozi wetu aliye fufuka atatushindania. Ingawa mili zetu zinakuwa dhaifu, roho zetu sinafanywa upya kila siku. Katika mtazamo wa umilele, majaribu amaayo tunakumbana nazo kwa sasa kwa kuwa waaminifu kwa Yesu katika ulimwengu ambao ni hatari, itaonekana sio kitu tukilingalinsa na utukufu wa milele ambao unatungojea sisi. Kwa hivyo, tunalenga macho yetu juu ya vitu ambavyo ni vya uzima wa milele-ambayo ni Kristo na utukufu ambao ametushindania.

### **Vipengele vya kuzingatia**

1. Mbona ni ya muhimu kwetu sisi kutangaza wazi kuwa tuko chini ya Agano Jipya?
2. Ijili imefunikwa na adui huwapovusha watu ukweli. Ni kwa njia gani tunatafuta kubadilisha haya na kuleta changamoto kwa kazi ya adui, ili watu waweze kumuona Yesu jinsi alivyo kwetu sisi?
3. Injili ni Nuru. Ni kwa njia gani tunajaribu kushinda kiza katika ulimwengu?
4. Pingamizi ambazo Paulo alikumbana nazo zilikuwa kuu. Ni pingamizi gani wewe kama muamini ulikumbana nayo na ni kwa njia gani uliweza kushinda?
5. Ni nini sababu ambazo zilimfanya Paulo kuwa na uhakika kwamba hatustahili kufa moyo?

Mungu Akubariki

Richard Brunton